

**HALMASHAURI YA WILAYA SINGIDA**  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Singida.  
Simu Na. 0262502252/2237  
Fax: 0262502719  
E-Mail: ded.singidac@singida.go.tz



S.L.P. 27,  
SINGIDA

06/11/2018

## **TANGAZO LA KOTESHENI**

**KWA AJILI YA KUPATA MAFUNDI WA UJENZI WA NYUMBA YA  
KUHIFADHIA MAITI , JENGO LA KUFULIA, JENGO LA  
MAABARA, NYUMBA YA MGANGA, JENGO LA UPASUAJI NA WODI  
YA WAZAZI KATIKA KITUO CHA AFYA MSANGE**

- 1 Halmashauri ya Wilaya ya Singida imepatiwa fedha na Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Msange kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
- 2 Halmashauri ya Wilaya ya Singida inakaribisha maombi kwa mafundi wa kawaida wenye uzoefu kwa ajili ya ujenzi wa *Nyumba ya Mganga , jengo la Kufulia, Nyumba ya kuhifadhia maiti, Jengo la Maabara, Jengo la upasuaji na Wodi ya wazazi katika kituo cha afya Msange*
- 3 Maombi yawasilishwe katika nyaraka halisi moja pamoja na nakala (vivuli) 2 Katika Ofisi ya Katibu wa Kituo cha Afya Msange. yakiwa yamefungwa vizuri kwa umakini katika bahasha na kutaja anuani ifuatayo;  
KATIBU,  
KITUO CHA AFYA MSANGE,  
S.L.P 27, SINGIDA.
- 4 Aidha katika kukamilisha kazi hii fundi mwenye sifa zifuatazo atahitajika.
  - a) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kwenye shughuli za ujenzi (uzoefu kwenye ujenzi wa majengo ya serikali ni sifa ya

- ziada) ambatanisha nakala ya mikataba ya kazi zilizopita zinazofanana na kazi hii kama ulishawahi kufanya.
- b) Awe na uwezo mkubwa wa kusoma na kutafasiri ramani/michoro wa jengo husika
  - c) Awe anamiliki mafundi wasaidizi atakaosaidiana nao wasiopungua wanne.
  - d) Awe na vifaa vyote muhimu vya ujenzi. (vifaa vya kufanyia kazi)
  - e) Apatishe maombi yake ofisi ya serikali ya Mtaa/Kijiji anachotoka.
- 5 Waombaji wenye nia watapatiwa maelezo ya kina na kupatiwa nyaraka za nukuu ya bei (Quotation) kutoka kwa Katibu, Ofisi ya kituo cha afya Msange SLP 27 Singida kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri siku ya Jumatatu hadi Ijumaa bila kujumuisha siku za mapumziko za Kitaifa.
- 6 Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **12/11/2018** saa **4:00 asubuhi siku ya Jumatatu** na kufuatiwa na ufunguzi utakaofanyika saa **4.30 asubuhi siku hiyohiyo** katika ukumbi wa **Kituo cha afya Msange**. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa kotesheni hizo. (Maombi yataambatana na ada ya zabuni kiasi cha **30,000/=** ambayo haitarudishwa)
- 7 Kotesheni zitakazoletwa zimechelewa, au zitakazotumwa kwa mtandao (fax or email) hazitofunguliwa na zitarejeshwa kwa wahusika.

Imetolewa na:-



.....  
Rashid M. Mandoa

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA**